# ARUSHA
## FURSA LUKUKI

#Endless Opportunities

**Toleo la Mtandaoni: 03  Tarehe 16/12/2022**

#Kazi Iendelee

**UTALII, KILIMO, BIASHARA  NA UZALISHAJI**

# PONGEZI MHE RAIS

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DKT SAMIA SULUHU HASSAN AKIWA KWENYE PICHA YA PAMOJA NA RAIS WA MAREKANI JOE BIDEN MARA BAADA YA KUWASILI KATIKA IKULU YA MAREKANI JIJI-NI WASHINGTON D.C. TAREHE 14/12/2022. KULIA NI JILL BIDEN MKE WA RAIS WA MAREKANI JOE BIDEN.**

# WAZIRI KAIRUKI ATANGAZA WALIO FAULU MTIHANI WA ELIMU MSINGI.

**“Jumla ya wanafunzi 1,073,941 wameshaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza Mwaka 2023”.**

**Akisoma taarifa hiyo kwa waandishi wa habari, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Angellah Kairuki amesema wanafunzi hao wote wanatakiwa kuanza masomo yao ya kidato cha kwanza mapema Januari 9, 2023.**

**Amesema idadi hiyo imejumuisha wavulana 514,846 na wasichana 559,095 ikiwa ni ongezeko la ufaulu wa wanafunzi 166,139 sawa na 18.3% ambapo kwa mwaka 2022 waliojiunga na kidato cha kwanza walikuwa 907,802.**

**Miongoni mwa waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wapo wanafunzi wenye mahitaji maalumu 2,775 sawa na 0.26% ikijumuisha wavulana 1,491 na wasichana 1,284.**

**Mhe.Kairuki amewataka wanafunzi wote waliopangiwa shule za bweni 4,224 kulipoti shuleni ifikapo Januari 7,2023 na wale wa shule zautwa 1,069,717 sawa na 99.61% kulipoti shule ifikapo Januari 9,2023.**

**Vilevile, ameagiza uwandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza kukamilika ifikapo Disemba 31,2022.**

**Aidha, amewaagiza Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi kuhakikisha miundombinu yote ya shule inakamilika ifikapo Disemba 24,2022 ili kuruhusU wanafunzi wa kidato cha kwanza kuanza masomo yao mapema Januari 2023.**

# UZINDUZI WA MITAALA YA ELIMU MAALUM, CHUO CHA UALIMU ELIMU MAALUM PATANDI.

**Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Angellah Kairuki amewaagiza Maafisa Elimu Maalum wote Nchini kuhakikisha wanasimamia zoezi la uchunguzi wa awali wa watoto ili kubaini watoto wenye mahitaji maalum katika jamii.**

**Ameyasema hayo hivi karibuni wakati akifungua mafunzo kwa Maafisa Elimu Watu Wazima na Maafisa Elimu Maalum iliyofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Ualimu Patandi, Mkoani Arusha.**

**Amewataka kuhakikisha wanatumia Vituo vya uchunguzi (Education Support Resource Assessment Centre) na kuwaelekeza watoto wenye mahitaji maalum katika shule stahiki ambazo wanapaswa kupelekwa ili wapate afua stahiki**

**Waziri Kairuki ameelekeza shughuli za usimamizi na uendeshaji wa Elimu zihusishe kikamilifu masuala ya Elimu Maalumu na Elimu ya Watu Wazima kwa kuhakikisha wanashirikiana na Viongozi katika jamii kuratibu shughuli za Elimu ya Watu Wazima na Elimu za Msingi na Sekondari.**

**Ametoa rai kwa Maafisa hao kuweka utaratibu wa kupokea Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum wa kidato cha kwanza, darasa la kwanza na awali kwa mwaka 2023 kwa kushirikiana na Viongozi katika maeneo yao ili kuweka mazingira bora kwa wanafunzi hao.**

**Waziri Kairuki amewataka Viongozi wa Elimu katika ngazi ya Shule, Kata, Halmashauri na Mikoa kufuatilia ufundishaji na ujifunzaji Shuleni kwakushirikiana na Walimu katika kuhakikisha Wanafunzi wanapata umahiri uliokusudiwa badala ya kukaa ofisini.**

**Aidha, ameagiza kila mwalimu ajiwekee malengo binafsi katika masomo anayofundisha na kuhakikisha hakuna mwanafunzi anayeshindwa kupata umahiri uliokusudiwa katika somo lake ifikapo mwishoni mwa kila mwaka.**

# WAZIRI AWATAKA VIONGOZI WA MIKOA NA HALMASHAURI KUSIMAMIA ELIMU YA AWALI NA MSINGI (BOOST)

**Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe. Angellah Kairuki amewataka wataalamu kutoka ngazi za**
**Mikoa na Halmashauri kwenda kusimamia Miradi ya kuboresha na kuimarisha elimu ya Awali na Msingi (BOOST) kwa kufuata Miongozo, Sheria na Kanuni zilizowekwa.**

**Ameyasema hayo, alipokuwa akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo Wataalamu mbalimbali kutoka ngazi za Mikoa na Halmshauri kwa kanda ya Kaskazini, yaliyofanyika kaika Shule ya Sekondari Iliboru-Arusha.**

**Mradi wa BOOST umelenga kujenga madarasa 12,000 kwa Nchi nzima na Shule salama takribani 1000 ,huku ukilenga kuongeza uwandikishaji wa Wanafunzi Shule za awali na pia, wahakikishe afua zote za mradi zinatekeleza kwa wakati ikiwemo miundombinu ya Shule.**

**Aidha, amesisitiza katika utunzaji wa nyaraka za miradi yote na kuwataka wataalamu hao kuiandika vizuri ili kutunza kumbumbuku.**
**Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI Ramadhani Kairima amesema kwa kanda ya Kaskazini jumla ya wanafunzi wakufunzi 274 watajengewa uwezo wa mradi huo.**

**Kairima amezitaka Halmashauri zote kuufanya mradi huo kuwa agenda ya kudumu katika vikao vyao. Mradi BOOST umezinduliwa rasmi Mkoani Arusha ikiwa ni Kanda ya Kaskazini iliyojumuisha Mikoa ya Manyara, Kilimanjaro, Singida na Arusha .**

OFISI YA MKUU
WA MKOA
ARUSHA

*#Utalii Fahari Yetu*

**Waziri OR-TAMISEMI Mhe. Angellah Kairuki akiteta jambo na Mkuu wa Mkoa Wa Arusha Mhe. John V.K Mongella katika uz-indzi wa Mitaala ya Elimu Maalum - Chuo cha Patandi.**

**Waziri OR-TAMISEMI Mhe. Angellah Kairuki akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John V.K Mongella wakiwa katika ukaguzi wa Mradi wa Sequip Shule ya Sekondari KIUTU-Arusha DC.**

OFISI YA MKUU
WA MKOA
ARUSHA

*#Utalii Fahari Yetu*

**WAZIRI WA NCHI,OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU PROF. JOYCE NDALICHAKO AKIWA KATIKA PICHA YA PAMOJA NA BI. FATMA MACHAKU AMBAYE NI MLEMAVU WAKATI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA WALEMAVU DUNIANI. TAREHE 03/12/2022**

**Katibu Tawala Mkoa wa Arusha  Bw.Missaile Musa akitoa zawadi kwa wanafunzi katika Maadhimisho ya Siku ya kupinga Ukatili wa Kijinsia na Ukatili dhdi ya Watoto Duniani.**

# MAADHIMISHO YA KUPINGA UKATILI WA KIJINSIA

**“Serikali haipingi Mila na Desturi bali haitafumbia macho zile Mila na Desturi zinazoleta Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto”.**

**Hayo yamesemwa na Katibu Tawala Mkoa wa Arusha Missaile Musa katika kilele cha siku 16 za Maadhimisho ya kupinga Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto yaliyofanyika katika Viwanja vya TBA Jijini Arusha.**

**Matukio ya Ukatili wa Wanawake na Watoto bado yapo kwa kiwango kikubwa katika Mkoa wa Arusha kwani kwa mwaka 2021/2022 jumla ya matukio 4705 yalilipotiwa na kati ya hayo matukio 4013 yalikuwa ya Wanawake na 692 ni Wanaume na ndani yake yakiwepo ya Watoto.**

**Aidha,katika mwaka 2019 jumla ya matukio 2339 yalilipotiwa ikiwa ni pungufu ya mwaka 2022 ambayo yalikuwa 4706 na hii imetokana na watu kupata uelewa wa kutoa taarifa kwa Mamlaka husika juu ya matendo hayo ya ukatili.**

**“ Naziagiza Kamati za MTAKUWA kuanzia ngazi ya Vijiji hadi Halmashauri zifanye kazi na kila Halmashauri ianzishe kituo cha Mkono kwa Mkono kwenye Hospitali za Wilaya ili kuhakikisha vitendo vya ukatili vinatokomezwa’, alisema Bwana Musa.**

**Kwa upande wake Afisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Arusha, Bwana Denis Mgiye amesema vitendo vya ukatili vinavyoongoza ni ukatili wa kimwili,kisaikolojia,kingono, mimba na ndoa za utotoni, ukeketaji na kushindwa kutoa malezi kwa watoto.**

**Hata hivyo, amewahasa Wanaume kujitokeza kwa wingi kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia kwani wameonekana wapo nyuma wakati vitendo vya ukali wanafanyiwa.**

**Nae, Afisa ustawi wa jamii kutoka kituo cha Mkono kwa Mkono cha Hospitali ya Mt.Meru Daniel Kasikiwe amesema wahanga wengi wamejitokeza kutoa taarifa za ukatili na hiyo imewezekana baada ya elimu kuendelea kuwafikia wananchi.**

**Aidha, amesema bado kuna changamoto ya wahanga kuchelewa kutoa taarifa ndani ya masaa 72 na hivyo kusababisha kupotea kwa ushahidi na baadhi ya wahanga kutotoa ushahidi pindi kesi inapofika mahakamani.**

**Maadhimisho ya kupinga ukatili wa kijinsia na watoto yalianza Novemba 27 na yamemalizika Disemba 10 katika Mkoa wa Arusha ambapo utoaji wa elimu ulifanyika katika kila halmashauri kwa kupita kwenye mashule, vyuo na makundi mbalimbali ya wananchi.**



# KIKAO CHA WADAU WATUMIA MAJI NA EWURA–ARUSHA

**Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongella ameuwagiza Uongozi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (AUWSA) kuhakikisha wanatoa huduma bora na endelevu baada yakufanya mabadiliko ya bei za Maji.**

**Ameyasema hayo alipokuwa akifungua kikao cha wadau na watumiaji wa Maji Mkoani Arusha wakati wa kujadili mapendekezo ya mabadiliko ya bei za Maji katika Jiji la Arusha kilichosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Kanda ya Kaskazini (EWURA).**

**”Mkikubaliana kufanya haya mabadiliko ya bei za Maji,AUWSA hakikisheni mnatoa huduma bora na endelevu kwa Wananchi”. Kazi kubwa ya Serikali hivi sasa ni kuwekeza kwenye miundombinu ya utoaji huduma bora kwa wananchi wake hususani zile huduma za muhimu zaidi kama vile maji,hivyo jukumu hilo Serikali imelikasimu kwa Mamlaka zake za Maji ikiwemo Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha(AUWSA)pamoja na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).**

**Pia,Mongella ameitaka mamlaka hiyo kuendelea kuboresha miundombinu na mtandao wa Maji ili huduma hiyo iweze kuwafikia Wananchi wengi kwa haraka zaidi na kwa kuzingatia usafi mazingira.**

**Aidha, amewahasa Wananchi kuchangia mjadala huo kwa uhuru ili waweze kuweka uwiano wa mawazo yatakayosaidia kuboresha huduma hiyo ya Maji kwa kiasi kikubwa.**

**Naye Meneja wa Kanda ya Kaskazini kutoka Mamlaka ya udhibiti wa huduma za Nishati na Maji (EWURA) Mhandisi Lorivil Long’idu, amesema baada ya kupokea maombi ya marekebisho ya bei za Maji na Usafi wa Mazingira kutoka AUWSA walifanya tathimini ya kina na kuona kuna umuhimu wa kufanya marekebisho hayo.**

**Vilevile amesisitiza kuwa mfumo unaotumika ni kuwashirikisha wadau na watumiaji wa Maji ili kupata maoni yao ya namna yakuboresha huduma hiyo kwa faida za pande zote mbili ikiwemo mtoa huduma (AUWSA) na Wananchi.**

**Kikao hicho cha siku moja kilijumuisha Viongozi mbalimbali, Wananchi na wadau wa Sekta ya Maji Jijini Arusha.**